# UQAB

Jarida la Uqab

Toleo 6

Julai 2017 MILADI

Shawwal 1438 Hijria



Tangazo la Muandamo wa Mwezi wa Shawwal

Demokrasia: Tumekomeka!


Safaricom, Dola, Ufalme au Jamhuri?

Je, Ulijichagulia


'MAMA' Wasiyewahi Kuwa naye...

Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi Halaqa 2

Mgogoro Baina ya Saudi Arabia na Qatar?


## Ujumbe wa Ameer wa Hizb ut Tahrir, mwanachuoni mkubwa Ata Bin Khalil Abu al-Rashtah kwa wenye kuzuru machapisho yake kwa tukio la kufikiwa na Eid al-Fitr iliobarikiwa Mwaka wa 1438 Hijria/2017 Miladi




بسم الله الرحمن الرحيم

**[Bismillah Al-Rahman Al-Raheem]**

**Ujumbe wa Ameer wa Hizb ut Tahrir, mwanachuoni mkubwa Ata Bin Khalil Abu al-Rashtah kwa wenye kuzuru machapisho yake kwa tukio la kufikiwa na Eid al-Fitr iliobarikiwa Mwaka wa 1438 Hijria/2017 Miladi**

Sifa njema ni zake Allah (swt) na Sala na salamu zimfikie Mtume (saw), Familia yake, masahaba zake na wote wanaomfuata…

Kwa Ummah wa Kiislamu uliotukuzwa na Allah (swt) aliposema:

**[كُنْتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِالْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ]**

"Nyinyi mmekuwa bora ya umma walio tolewa watu, kwa kuwa mnaamrisha mema na mnakataza maovu, na mnamuamini Mwenyezi Mungu. Na lau kuwa Watu wa Kitabu nao wameamini ingeli kuwa bora kwao. Wapo miongoni mwao waumini, lakini wengi wao wapotovu" [Aali-Imran: 110]…

Kwa wabebaji da'awa wasafi na wachamungu, na hatusifu mtu yeyote kwa Mwenyezi Mungu, wale ambao husema maneno bora na kufanya kazi njema, ambapo Mwenyezi Mungu huwasifu wale ambao wana sifa hizo:

**[وَمَنْ أَحْسَنُ قَوْلًا مِمَّنْ دَعَا إِلَى اللَّهِ وَعَمِلَ صَالِحًا وَقَالَ إِنَّنِي مِنَ الْمُسْلِمِينَ]**

"Na ni nani mbora wa kusema kuliko aitaye kwa Mwenyezi Mungu na akatenda mema, na akasema: Hakika mimi ni katika Waislamu?" [Fussilat: 33]…

Kwa wageni watukufu wenye kuzuru kurasa za wavuti, kuzipitia kwa uaminifu na ukweli na kwa wale wanaotafuta mema ambayo zimebeba kurasa hizi, Allah awalipe kwa yalio bora zaidi ...

Kwa hawa wote, nawapa pongezi kwa Eid al-Fitr na namuomba Allah (swt) akubali Swaum zao na Qiyam na kuwafanya miongoni mwa waliokombolewa katika mwezi huu Mtukufu. Na pia namuomba Mwenyezi Mungu Mwenye Nguvu kwamba hii Eid iwe mwanzo wa baraka na ustawi kwa Waislamu ili tuweze kufurahia Eid zifuatazo chini ya kivuli cha Rayah ya Khilafah Rashidah, bendera ya 'La Illaha Illah Allah Muhammadan Rasul Allah', na kwa kweli hiyo sio ngumu kwa Allah ...

Mwishowe nawatolea salaam na kuwaombea uzima wenu, Mwenyezi Mungu awatakabalie matendo yenu na awahifadhi kutokana na madhara na maovu yote.

**[فَاللَّهُ خَيْرٌ حَافِظًا وَهُوَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ]**

"…Lakini Mwenyezi Mungu ndiye Mbora wa kulinda, naye ndiye Mbora wa kurehemu kuliko wenye kurehemu wote." [Yusuf: 64].

Usiku wa Eid, 1 Shawwal 1438 Hijri / 25-6-2017 Miladi

**Ndugu yenu,**
**Ata Bin Khalil Abu al-Rashtah**


Email: uqab@hizb.or.ke

# Tangazo la Muandamo wa Mwezi wa Shawwal Mwaka wa 1438 Hijria na Pongezi za Siku Kuu ya Eid ul-Fitr al-Mubarak

**Allahu Akbar, Allahu Akbar, Allahu Akbar, La Ilaha Ila Allah, Allahu Akbar, Allahu Akbar, Wa lillah Alhamd**

Sifa njema zote ni kwa Allah na rehma na amani zimuendee Mtume wa Allah (saw) na jamaa zake na maswahaba zake na yule anayemfuata yeye na njia yake, na akaifanya Aqeedah ya Kiislamu msingi wa imani yake, na sheria za Kiislamu kuwa kipimo cha amali zake na chimbuko la kanuni zake…

Imepokewa na Ahmad kutoka kwa Muhammad Bin Ziyad, asema: Nimemskia Abu Hurairah akisema: Mtume (saw) amesema – au akisema Abu Qasim amesema:

«صُومُوا لِرُؤْيَتِهِ، وَأَفْطِرُوا لِرُؤْيَتِهِ، فَإِنْ غُبِّيَ عَلَيْكُمْ فَعُدُّوا ثَلَاثِينَ»

((Fungeni kwa kuonekana kwake (muandamo wa mwezi wa Ramadhan), na fungueni kwa kuonekana kwake (muandamo wa mwezi wa Shawwal), ikiwa mawingu yatatanda juu yenu (kiasi cha kutoweza kuuona mwezi), basi hesabuni (siku) thelathini.))

Baada ya kuutafuta muandamo wa mwezi wa Shawwal katika usiku huu wa kuamkia Jumapili, muandamo wake umethibitishwa kuambatana na matakwa ya kisheria ya muandamo wa mwezi katika baadhi ya biladi za Waislamu, hivyo basi kesho, Jumapili ndio siku ya kwanza ya mwezi wa Shawwal na ndio siku ya kwanza ya Eid ul-Fitr al-Mubarak.

Katika Siku Kuu hii ya Eid ul-Fitr al-Mubarak, Amiri wa Hizb ut Tahrir, mwanachuoni maarufu Ata Bin Khalil Abu Rashtah, Allah amuhifadhi, anawapongeza watu wote katika umma huu mtukufu wa Kiislamu, na anamuomba Allah Subhanahu kuturuzuku fadhla yake kwa kusimamisha Khilafah Rasheedah katika njia ya utume itakayo tekeleza Sheria za Allah duniani na kubeba Uislamu kama ujumbe wa uongofu na nuru. Dola ya uadilifu itakayo komboa ardhi na kuleta haki kwa watu; dola ya Jihad itakayo endeleza ufunguzi wa miji, na watu watapiga takbira katika Eid zao, na Futuuhaat zao: Allahu Akbar, Allahu Akbar, Allahu Akbar, la ilaha illa Allah, Allahu Akbar, Allahu Akbar, Wa lillah Alhamd

Ni furaha yangu pia kutuma pongezi zangu na za kiongozi wa afisi kuu ya habari ya Hizb ut Tahrir na wale wote wanaofanya kazi ndani yake, kwa Amiri wa Hizb ut Tahrir, na kwa Waislamu wote kwa Eid hii al-Mubarak; hii ni Siku Kuu ambayo Allah ameituma ili iwe furaha kwa wenye kufunga na ishara ya umoja kwa Waislamu, na ukumbusho kwao kwamba wao ni Ummah Mmoja tofauti na wengine.

**Enyi Waislamu:**
Namuomba Allah (swt) akubali kutoka kwenu na kwetu saumu na qiyam, rukuu na sujud na amali zote njema. Kama pia ninavyo muomba arudishe juu ya Umma wa Kiislamu uwepo wa Khaleefah muongofu, utakao hifadhika kutokana naye na kupigana nyuma yake, na kuwahukumu kwa kitabu cha Allah na Sunnah za Mtume wake (saw), na hilo ni jepesi kwa Allah.

**Eid ul-Fitr ni fadhla kutoka kwa Allah Azza Wa Jal juu ya Waislamu, na Eid hii kati ya Eid zote ndio ambayo ahadi ya Allah na bishara za Mtume wa Allah (saw) zinapotimia kwa ushindi na utawala, na kuunda serikali inayo hukumu kwa sheria za Allah, Khilafah Rasheedah katika njia ya utume.**

Ili furaha hii ikamilike, ni lazima tuzing'oe serikali za kibinadamu, vibaraka wa makafiri na wakoloni, wasaliti wa Allah, Mtume wake na Waumini wake.

Ili furaha hii ikamilike, ni lazima nguvu zote za Ummah wa Kiislamu ziunganishwe pamoja.

Ili furaha hii ikamilike, majeshi ni lazima yawape nusra wale wanaofanya kazi kwa ikhlasi kuleta ushindi wa Uislamu.

Ili furaha hii ikamilike, hapana budi kuregea tena kwa maisha kamili ya Kiislamu katika kila nyanja za maisha: kisiasa, kiuchumi, kijamii, na kielimu.

Ili furaha hii ikamilike, jengo kubwa la Kiislamu ni lazima lijengwe, nalo ni Khilafa Rasheedah ya pili katika njia ya utume.

Nawakaribisha kutimiza lengo la Eid hii na Eid zote, fanyeni kujifunga na sheria za Allah (swt) kuwa ndio hatma ya Eid yenu, kupitia kufanya kazi na wafanyi kazi wenye ikhlasi kuleta ushindi na utawala kwa dini hii na kupiga takbira kwa pamoja siku hiyo ya ushindi, takbira za washindi, watiifu, wenye kumsifu Allah na kuomba msamaha wake.

**Allahu Akbar, Allahu Akbar, Allahu Akbar, La Ilaha Ila Allah, Allahu Akbar, Allahu Akbar, Wa lillah Alhamd**
**Allahu Akbar Kabira, Walhamdulillah Katheera, Wa Subhan Allah Bukratan Wa Aseela**
**La ilaha illa Allah, Wahdahu, Sadaqa Wa'dahu, Wa Nasara Abdahu, Wa A'azza Jundahu, Wa Hazzam Al Ahzab Wahdahu**
**La Ilaha Illa Allah… Wa la Na'budu Illa Iyyahu…Mukhliseen Lahu Ad-Deen Wa Lau Kariha Al-Kafiroon**

Eid Mubarak na Allah atakabali kutoka kwenu na kwetu amali njema

Wassalamu Alaikum Wa Rahmatullah Wa Barakatuhu

Usiku wa Eid, 1 Shawwal 1438 Hijri / 25-6-2017 Miladi

**Dkt. Osman Bakhach**
**Mkurugenzi wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**



# DemokrasiaTumekomeka!

Imesalia miezi miwili tu kuingia kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu 2017. Huu utakuwa ni uchaguzi wa bunge la kumi na mbili na kama ilivyo ada miungano ya kikabila chini ya mwavuli wa vyama vya kisiasa imebuniwa huku vigogo wa miungano hiyo wakimwaya pesa wakidanganya watu kwa kuwasihi kushiriki kwenye uchaguzi. Kabla hata ya uchaguzi huu tayari uchafu wa Demokrasia ulihisika kwenye mchakato wa uteuzi uliokumbwa na uhuni,ghasia na mauaji! Bila shaka hii ilikuwa ni chachu ya Demokrasia ambayo kiuhalisia imeshindwa kuunganisha jamii bali ni siasa ya ulafi,ukabila na ufisadi.

Kwa jamii ya Kiislamu, uchaguzi huu unakuja baada ya miaka kadhaa ya oparesheni kadhaa za polisi dhidi ya Waislamu na kupotea kwa vijana wengi wa Kiislamu mikononi mwa jeshi la polisi katika maeneo yenye idadi kubwa ya Waislamu kama vile Pwani na kaskazini Mashariki. Jijini Nairobi, wakaazi wa Eastleigh wanakumbuka kwa machungu dhulma ya kutolewa majumbani mwao na kuwekwa katika uwanja wa Kasarani huku wakipigwa na baridi kali kwenye operesheni 'Usalama Watch'. Licha ya hayo, mikakati kadhaa ya kiserikali kwa msukumo wa dola kuu za kimagharibi ya kuwalazimisha Waislamu kuachana na Uislamu wao imeshika kasi katika kile kiitwacho vita dhidi ya misimamo mikali na itikadi kali.

Kwa hivyo uchaguzi huu unakuja katika kipindi ambacho Waislamu wanajiuliza maswali mengi juu ya mustakabala wao. Licha ya kuweko baadhi ya viongozi wa Kiislamu wakihimiza watu haja ya kupiga kura lakini kihakika mwito wao huu unakabiliwa na upinzani mkubwa kwa Waislamu ambao kwa sasa ni waathiriwa wakubwa kwenye vita dhidi ya ugaidi. Sio hilo, hata ahadi za Wabunge Wakiislamu na vyama vyao walivyoegemea zote zimefeli katika kutetea maslahi ya Waislamu kikweli hivyo basi Waislamu wamejipata hali mbaya zaidi.
Japo kuwa uchaguzi wenyewe bado miezi kadha lakini tayari joto lake twalihisi. Hali hii ikiingia basi kila kilichobaki hakina umuhimu au kina chukua nafasi ya nyuma ya suala zima la uchaguzi. Wakati huu masuala kama ya Uchumi, Elimu, Matibabu, Usalama na hata majanga kama ya Ukame, mafuriko na migomo kama ya madaktari huchukua nafasi ya nyuma, yakitanguliwa na suala la uchaguzi. Na yakiangaziwa basi huwa kwa mazingira ya kutafuta umaarufu kwa lengo la kushinda uchaguzi huo.

Basi kwa nini hatujifunzi kutokana na yale yanaojirudia kila misimu ya uchaguzi? Bali swali la kuulizwa ni kwa nini tunga'ng'anie nidhamu hii ya kisiasa ya kidemokrasia inayotutia kitanzi cha koo kabla ya uchaguzi, wakati wa uchaguzi na baada ya uchaguzi? Kwani hatuoni kadri siku zinavyosonga hali yazidi kudorora kwa mwananchi wa kawaida ilihali twashiriki katika uchaguzi tukiwa na tamaa ya kuleta mabadiliko?
Kila wakati wa uchaguzi twashiriki kwa kisingizio imma kwa khofu kuwa kutoshiriki kwetu hali itakua mbaya zaidi (kuliko hii!?) au twatiwa tamaa kushiriki kutapatikana mabadiliko, (tamaa ya mazagizagi!?).

أَفَحُكْمَ الْجَاهِلِيَّةِ يَبْغُونَ وَمَنْ أَحْسَنُ مِنَ اللَّهِ حُكْمًا لِقَوْمٍ يُوقِنُونَ

Je, wao wanataka hukumu za Kijahiliya? Na nani aliye mwema zaidi katika
kuhukumu kuliko Mwenyezi Mungu kwa watu wenye yakini? [Al Maida:50]

**Hizb ut-Tahrir Kenya** imebainisiha mara kwa mara hukumu ya kisheria juu ya kushiriki kwenye chaguzi za Kidemokrasia. Kwa kuwa huu ni wajibu wa kila muislamu basi hatutochoka kurudia kuweka wazi hukmu hii licha ya wengi ya Waislamu kujitia uziwi na upofu mbele ya haki. Suala la uharamu wa kushiriki katika uchaguzi wa kidemokrasia uko wazi katika Muongozo wa Allah swt. Lakini kwanza twataka tuweke suala hili la uharamu wa kura wazi, tukisema kura ni haramu katika nidhamu ya kidemokrasia ni kwa sababu ya lile lengo lililowafanya watu washiriki katika uchaguzi huo nalo nikumchagua kiongozi atakaehukumu na ukafiri au kuwachagua watu watakao kwenda kutunga sharia. Kwetu sisi Waislamu ni jambo linalojulikana kuwa sheria ni za Mwenyezi Mungu SWT pekee na kuwa wanadamu wanapaswa kupeleka maisha yao kwa mujibu wa sheria hizo.

إِنِ الْحُكْمُ إِلَّا لِلَّهِ

Hapana hukumu ila ya Mwenyezi Mungu tu.[Yusuf:40]

Uchaguzi/kura katika Uislamu ni mubah lakini inapokua uchaguzi unafanywa kwa misingi inaogongana na Itikadi yake au Sheria zake basi Allah swt ametukataza kushiriki.
Nidhamu ya kidemokrasia ni nidhamu ya kisiasa katika mfumo wa kirasilimali uliochipuka kutoka katika itikadii ya ki'ilmani- kutenganisha dini na maisha na kwa kuwa Muumba na Sheria zake ametengwa kutoka katika maisha ya mwanadamu, jukumu la kutunga sheria zitakazo muongoza katika maisha yake hapa ulimwenguni limepewa mwanadamu mwenyewe na akili yake finyo. Mwanadamu kwa mujibu wa akili

*Endelea Uk..5*



Email: uqab@hizb.or.ke

yake atachagua kipi kizuri na kipi kibaya na hubadilika haya kwa mujibu ya maeneo, mazingira, wakati, dhurufu na hali… Kwa hivyo jambo laweza kusemwa kuwa ni zuri kisha likabadilika kuwa baya na kinyume chake kwa kuathiriwa na maeneo, wakati… ukizingatia kuwa maslahi ndio kipimo cha maisha ndani ya mfumo huu. Amma katika Uislamu kizuri na kibaya ni kwa mujibu wa sheria za Allah, kwa hivyo haibadiliki wala kuathiriwa na humtatulia mwanadamu matatizo yake popote alipo na nyakati zote. Huku kumpa mwanadamu uweza wa kutunga sharia ni athari ya fikra ya kutenganisha dini na duniya ambayo inagongana moja kwa moja na fikra ya kumpwekesha Allah swt. Isitoshe itikadi hii ya ki'ilmani ndio iliompa huyu mwanadamu ubwana wa kujitungia sharia ambao ni ukafiri. Basi vipi Muislamu atashiriki katika uchaguzi huo wakuwapeleka watu imma kuhukumu kinyume na sheria za Allah au kutunga sharia kinyume na Allah swt? Kushiriki huku kwa kisingizio chochote ni kutambua ubwana wa mwanadamu kinyume na Allah swt na hili ni haramu hakuna shaka ndani yake.

**Enyi Waislamu:** Jee hamuridhiki na kile kilichomteremkia mtukufu wa viumbe Mtume saw na kuwafikishieni na kilicho kamilika na kutimia katika neema zake Allah swt nao ni Uislamu!? Basi kwa nini mutake upotofu unaotokamana na akili finyu za wanaadamu wachache wasokuwa na maadili? Ni wajibu juu yetu kama Waislamu kuuamini na kuubeba Uislamu kama mfumo kamili wa kimaisha ulio na suluhisho zote za kimaisha na kuwalingania wasio kuwa Waislamu ili kuwakomboa walimwengu na madhila haya! Hili ni sahali ikiwa tutawalingania Uislamu kwa usafi wake kama mstari ulionyoka na kuonyesha kombo ya mfumo, unaotawala leo ulimwenguni, wa kirasilimali na nidhamu yake ya kidemokrasia kwani watu wamechoshwa nao illa hawana mbadala. Hakuna pahala hili hudhihiri wazi kama Bara Afrika na haswa hapa kwetu Kenya, kwani urasilimali umeifukarisha kiuchumi juu ya kuwa na utajiri mkubwa, kuangamiza kwa migawanyiko ya kikabila na vita visivyokwisha, kuendeleza ubepari kwa maslahi ya Marekani na Ulaya. Hakika jamii zimechoshwa na hali zilivyo illa hawaoni badala nyengine kwa kuenezewa sumu dhidi ya Mfumo safi wa Uislamu, basi ni juu yetu kuwalingania usafi huu kwao na kuwasimamishia hoja. Basi huwaje Waislamu wakawacha kheri hii na kujiingiza kwenye machafu ya kidemokrasia? Imma kwa kugombea, kulingania au kushiriki katika chaguzi hizi na kuutia nguvu kinyume na Uislamu, hatuoni tuna majibu ya kujibu mbele ya Allah swt siku haitomfaa mtu mali wala wana?

Mfumo wa kirasilimali na nidhamu yake ya kiutawala ya kidemokrasia haijaleta kheri yoyote tangu mwanzo kuingia kwake bara Afrika na haswa nchi ya Kenya ilipoletwa kimabavu na wakoloni wakiingereza kwa malengo ya kuwatenza nguvu wenyeji na kufyonza rasilimali zao. Na hali haijabadilika hata baada ya kuondoka kwa wakoloni hawa na kuwapa wenyeji uhuru bandia wa bendera lakini hali halisi ikabakia kuwa wao ndio waendeshaji wa nchi kwa kupanga siasa kwa maslahi yao. Illa walifaulu kuwafunga watu macho kwa kuwaonyesha kuwa sasa nchi ipo katika mikono ya watawala ambao ni wenyeji na maraia wana haki ya kuwachagua kila baada ya miaka kadha. Hadaa hii imefaulu kuwapa watu tamaa ya kirongo kiasi ya kuwa hawaoni kuwa ukoloni unaendelea kwa sura nyengine na wala hayo mabadiliko wanayoyatarajia hayatokuja ndani ya mfumo huu, bali ni danganya toto tu.

**Enyi Waislamu:** Mfumo huu wa kibepari wa kirasilimali umefeli ulimwengu mzima, hata katika ulimwengu wa kwanza na wanaofaidika nao ni wachache walioko mamlakani. Kinachoibakisha kutotoweka kwake ni nidhamu yake ya utawala ya kidemokrasia inayowapa watu tamaa ya kushiriki kuleta mabadiliko na mwanzo mpya ilhali ukweli unabakia kuwa huu mfumo hauwafai hata kuwasimamia wanyama licha ya mwanadamu! Sisi Waislamu tuna mfumo badala wa Uislamu na nidhamu yake ya utawala wa Khilafah inayo tokamana na wahyi kutoka kwa Allah swt. Mfumo wa haki utakao leta uadilifu kwa kumpangia mwanadamu mahusiano yake na wengine kwa mujibu ya maamrisho na makatazo yanayotoka kutoka kwa Yule alietuumba na kutujua udhaifu wetu na mahitaji yetu. Ni juu yetu kuufahamu Uislamu wetu kama mfumo wa maisha ulio na suluhisho kamilifu kwa mwanadamu na utakao leta utulivu katika mgongo wa ardhi na kuondoa ufisadi ulioenezwa na mfumo mpotovu wa urasilimali. Ni juu yetu sisi kuwafikishia wasio kuwa Waislamu mfumo wa Uislamu kuwa ni suluhisho kwa mwanadamu na kumuondolea takataka masikioni alojazwa nazo na propaganda za mabepari wanaotishiwa na Uislamu. Urasilimali umekufa lakini yahitajika Uislamu ukitangaze kifo chake watu wabumburike kutoka katika usingizi mnono uliowagubika. Hatuna tena sababu za kunyamaza tukitarajia mambo yatakwenda kubadilika bali ni juu yetu kuleta haya mabadiliko kwa njia aliotuonesha Mtume saaw, laa sivyo tutaendelea kudhalilika na siku ya qiyamah tukutane na adhabu ilio kali.

**Hizb ut tahrir Kenya** inawakumbusha Waislamu kutembea nayo katika kuleta mageuzi ya kihakika yatakayo wakomboa wanadamu na madhila ya ukoloni unougubika ulimwengu. Pia tuna walingania kila mwenye akili kuuangalia Uislamu kama mfumo badala utakao wapa suluhisho za kudumu na kuleta utulivu kwa mwanadamu badala ya kila muhula kubahatisha katika uchaguzi wa pata potea ukijua ndani ya moyo wako kitendo chako hakitoleta mabadiliko ya kweli.
Allah swt asema:

وَمَنْ أَعْرَضَ عَنْ ذِكْرِي فَإِنَّ لَهُ مَعِيشَةً ضَنكًا
وَنَحْشُرُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَعْمَى

Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu.
[Taha:124]

**Hizb ut-Tahrir Kenya**
**1 Shawwal 1438 Hijri**
**25 Juni, 2017 Miladi**

# Safaricom

## DOLA, UFALME AU JAMHURI?

Kuna msemo wa kibepari husema "Kopa dolari kutoka kwa benki, benki ikumiliki; kopa dolari bilioni kutoka kwa benki, benki uimiliki"

Ni funzo kutoka kwa utumizi uliovuliwa kutoka kwa umilkaji na kwa hali hiyo, Safaricom inaimiliki Kenya. Safaricom inatawala asilimia hamsini na moja ya uchumi, ikiwa na wateja zaidi ya milioni 23.3. Kuliweka hili katika muktadha, jumla ya idadi ya watu ni milioni 45.6 ikiwemo nguvu kazi (wenye uwezo wa kufanya kazi) milioni 17.7 na kukuwa kwa kiwango cha ukosefu wa ajira kwa aslimia 24.3 na jumla ya kiwango cha wateja msingi wa simu milioni 33.6 ...

**…Safaricom inamiliki (watu) milioni 23.3!**

Tukiiweka kwa sura nyengine, Safaricom inamiliki kama wanateja, zaidi ya nusu ya idadi ya watu wote na kwa takwimu nyingine zaidi ya 88% (88.25%) ya idadi ya watu wote wazima. Hii ni kusema Safaricom mkononi mwake mawasiliano ya sauti, fedha, akiba, shughuli (za kibinafsi na za kibiashara), maelezo ya mahali, na maalumati kamili ya watu (bio data) kwa asilimia 88% ya idadi ya watu wote wazima.

Jamii huwasiliana kupitia mtandao wa simu. Kwa sababu hiyo siasa ya kijamii sasa hudhihirishwa kupitia mitandao, na hivyo basi kuleta maana ya msemo "jamii ya mtandao (Network Society)". Umaarufu wako unapimwa kwa wafuasi wako utambulisho wako wa kijamii (social identity) unaokusanya. Mabadiliko haya yanaweza kuhisiwa kwa urahisi zaidi kutokana na umuhimu uliopindukia wa nambari yako ya simu ya rununu kuliko ile nambari ya kitambulisho chako ulicho pewa na serikali. Unahitajika hata kunakili nambari yako ya simu ya mkononi katika safu sambamba na ya kitambulisho chako katika kuingia maeneo yote yanaodhibitiwa.

Kando na hili, wakati swali lilipoulizwa ni haja gani au ni kusudio gani la kuwepo "ulazima" wa kujitambulisha huku, mwandishi aliwahi kujibiwa na bawabu katika meza, bila hata kuhisi kejeli kwamba,
"Ni kwa ajili ya manufaa yako mwenyewe. Kwa mfano, jengo likiporomoka tutajua jinsi ya kukufikia wewe."
Kwa kipimo hiki, Safaricom ni muamuzi msingi wa mahusiano yote ya kijamii na ya kiuchumi kwa wakazi wa nchi yote. Kituo kimehama, Safaricom ndio kituo kipya. Rais Uhuru Kenyatta anaendelea kupiga kelele yeye ni dhaifu, lakini hakuna wa kumsikiliza. Ikiwa kampuni ya United Food Company iliifanya Honduras na Guatemala "Jamhuri ya Ndizi (Banana Republic)" basi Kenya na mataifa mengine katika mkono wa Safaricom yana umuhimu kwake kuwa "Jamhuri ya safaricom". "Safaricom" kwa sababu Safaricom ni ya kipekee si tu kwa biashara, benki, mawasiliano ya sauti na ya maandishi, ufuatiliziaji wa usalama na burudani, lakini katika kina cha utawala wake katika suala la kufikia kwa idadi, bidhaa na uwezo wa kijamii na kisiasa.

Safaricom iko na ushawishi wa zana za kupima jamii za usuluhishi, nguvu na usimamizi pasi na mizani ya mamlaka ya kijamii na makosa yaliyotokea, na hapa ndipo penye tatizo. Kiufupi, swali tunalofaa kuuliza ni, Ili kurekebisha ubaguzi je, Bob Collymore avishwe taji la ufalme? Au Safaricom iraruliwe na kuangamizwa?

Safaricom ni taasisi halisia, kijamii na kiuchumi lakini si kisiasa. Kutokana na ukubwa kamili wa utawala wa Safaricom juu ya jamii, nadharia ya kisiasa inaonyesha ni lazima kubeba mzigo na changamoto za jamii na kiuchumi kwa usawa. Ada ya huduma ya M-Pesa kwa sifa yake ya kuenea kwake kila mahali na kutokwepeka (kwa kuwa huchukuliwa kutoka kwa zaidi ya asilimia 88 ya idadi ya watu wazima) ni kodi ya kiuchumi ya jamii nzima na ushuru wa kihakika. Safaricom ni hazina kwa zaidi ya asilimia 88 ya idadi ya watu wazima, kwa kuwa asili mia 88 haiwezi kuepuka kodi ya Safaricom, Safaricom hivyo basi ina wajibu wa kijamii na kiuchumi kwa hii asilima 88, ipitayo uhusiano mwema wa kijamii, usambazaji upya wa kirongo wa utajiri, mazoezi ya kiusanii kama hili la Jukumu la Ushirika kwa Jamii (CSR). Huku si kupoteza kwa Safaricom kama inaevyoeleza ripoti yake ya 'thamani ya kihakika' kwamba "thamani katika Jamii sasa imeunganishwa na thamani ya kikampuni ya

*Endelea Uk..7*



Email: uqab@hizb.or.ke

Safaricom".

Huku ikiwa ni kukatikiwa kwa uhakika kuwa si kweli kuwa mafanikio ya Safaricom kwa hali yoyote inapelekea mafanikio ya kijamii, kufeli kwa Safaricom ndio kiuhakika inapelekea kufeli kwa jamii katika kiwango kikubwa. Hii ni kwa sababu nchi hii na idara yake, kinyume na hadithi ya shirika la AIG na serikali ya Amerika, kamwe haiwezi kuhimili kufeli kwa Safaricom. Safaricom sio benki ya Imperial, benki ya Chase, shirika la ndege la Kenya Airways wala benki ya kitaifa (National Bank).

Faida ya shilingi bilioni 48 iliyotangazwa ni kama tutakavyoonyesha katika tolea lijalo, aghlabu imenukuliwa kwa uchache mno. Hesabu za kiudadisi za kiwango cha chini kabisa za ashiria kuwa faida baada ya kutoa gharama zote inagonga shilingi bilioni 60 (ikizingatiwa uzito wa gharama za uendeshaji wake, ondoa bilioni 5). Lakini kilicho muhimu kwetu kama jamii ni kuwa 'faida' hiyo ya shilingi bilioni 48 kiuhakika ni pato la ushuru. Huyu hakuwa afisa mkuu mtendaji anayetoa ripoti ya faida ya kibiashara, bali lilikuwa tangazo la mapato lililo tangazwa na kamishna mkuu wa hudumu ya ushuru. Ama kwa raia hakuna khiari yoyote katika kadhia ya ima kujisalimisha au kutojisalimisha kwa Safaricom. Kama ilivyo katika ushuru, kila mmoja lazima alipe isipokuwa mfalme.

Safaricom, kama ilivyo, Bob Collymore amefuzu kupata kiti katika kamati ya benki kuu inayoshughulika na sera za kifedha, kwa kuwa mtu pekee aliye tegemewa pakubwa katika mwendo kasi wa fedha. Bob Collymore pia ana uwezo wa kupata kiti katika baraza la kitaifa la usalama, kutokana na kuwa Safaricom ndio ishara msingi ya kijasusi na muundo msingi wa kiuchunguzi kwa idara ya nchi. Takwimu za kiuchumi za safaricom zaweza kuwa kipimo cha mkato cha harakati za kibiashara kwa wakati wowote sasa kinyume na mwanzoni. Hitilafu ya kimitambo ya safaricom ya mnamo Jumatatu 24 Aprili 2017 imedhihirisha kutawala kwake mambo ya kiuchumi katika upeo wa wastani. Barabara zote zilisimama, kuanzisha barabara ya Kirinyaga kuelekea mpaka barabara ya Juja hata pengine nchi nzima, kila raia na kila muamala, mpaka Bob Collymore akasubiri ushauri kutoka kwa timu ya kiufundi ya safaricom. Je kumkabidhi Bob Collymore nguvu hizi za kuunda sera zitakuwa kubwa zaidi kuliko zile alizo nazo sasa katika safaricom? Je zitalingana na 'thamani ya kihakika' ya safaricom?

Huku ukizingatia kuwa safaricom mara kwa mara hutukumbusha katika ripoti ya Safaricom KPMG 'ripoti ya thamani ya kihakika' kuwa 'thamani yao ya kishirika' na "thamani yetu ya kijamii' zina uhusiano, ulio maalum.
Kwa ufupi kubali kuwa, safaricom imeiteka Kenya.
Kuwa au kutokuwa … nini kufanya au kutofanya… hilo ndilo swali.

Ni muda gani ambao ungechukua kuanzia Jumatatu 24 Aprili 2017 kabla walala hoi eneo la Eastlands kulitembelea kasri la Collymore katika eneo la kifahari la Westlands? Wiki? Siku? Masaa? Je Safaricom ina badali gani? Ni taasisi au mkusanyiko wa taasisi gani ambazo zinaweza kuuchukua mpira ikiwa safaricom itauangusha? Ni nini… ni wapi ilipo feli safaricom? Kwa kuwa mwanadamu ni mkosefu, taasisi zina uwezo wa kufeli na ni muhimu kuelewa kwamba aliye hatarini zaidi ni mwanadamu na wala si teknologia…


Kenya yahitaji kuzingatia kwa makini katika kujisalimisha. Tuna bahati sana ni msimu wa uchaguzi. Kenya tayari imejitayarisha kwa mpito wa kisiasa. Je tuwe ufalme wa safaricom au jamhuri ya safaricom? Ki uhakika barabara ya Waiyaki yatakiwa iwe na msongamano mkubwa wa magari moja kwa moja mpaka katika kasri la safaricom. Huku mabwenyenye; vinara, magavana wote na wengineo wakiweka mlolongo kutoa heshima, kupokea ufadhili na kuchukuwa msaada (kugawanya upya utajiri) kuwalisha wanajeshi (wa kisiasa) na watu walio fazaika na njaa wanaolinda kambi za machifu.

Kupeleka mbele lengo hili la kimaumbile pasi na kuwa mdanganyifu juu maana yake, italeta hisia isiyo ya kawaida. Kuunganisha pamoja nchi, watu, idara na makampuni makubwa ya kitaifa na ya kimataifa, kuwa utawala wa kikampuni.
Safaricom
ni 'ufalme' ikizingatia idadi ya mataifa yalio mikononi mwake, lakini Kenya ikiwa ndio moyo wake mkuu inachukuwa haki ya kuwa 'ufalme wa katikati'. Itahitaji mizani ya Jacobin ya njama kati ya vyama vya CAK, COFEK, na COTU na vyenginevyo kuandaa mapinduzi ya kiwango cha juu kutupilia mbali ugandamizaji wa safaricom ya kutugeuza sisi 'jamhuri' yake. Lakini pia ufalme na kurithi kwake nguvu ya kisiasa kumepitwa na wakati… kwa hivyo, 'jamhuri' ya safaricom ndio hiyo!

Kwa hivyo, raia wenzangu samahani, wananchi tukomeke na sarakasi za demokrasia na kundi lake la mabwenyenye wachache. Tutangazeni safaricom kuwa jamhuri na tumteue Bob Collymore kuwa kiongozi wa jamii!

Itaendelea katika UQAB Toleo 7…In Shaa Allah

**Arkanuddin Yassin**
**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano**
**Hizb ut-Tahrir Kenya**



# Je, Ulijichagulia Jukumu Lako Katika Taasisi ya Maisha?

Mtu imara ni yule anayejenga suluki yake juu ya msingi wa maamuzi. Ameamua kujenga maisha yake juu ya mtazamo maalum. Kwa maana nyengine… amejifafanulia maana ya kuwepo kwake hapa duniani. Mwanadamu hujifungulia njia yake hapa duniani kwa msingi wa kuweka mtazamo wake juu yake. Huanza kwa kujibu maswali yafuatayo: "**Ni kwa nini niko hapa dunia?**" na "**Ni nini lengo la kuwepo kwangu hapa duniani?**"

Ikiwa mwanadamu atakosa kutoa jibu la wazi, kwa kukatikiwa kikamilifu, na akajifunga na kusimama imara juu ya maswali hayo, basi hataweza kutambua suluki ambayo ni madhubuti, iliyo simama imara, yenye kuzaa matunda au iliyo na maendeleo kwa mwanadamu huyu. Kamwe hata pata suluki itakayompeleka katika furaha anayoitafuta kutokana na umbile lake kama mwanadamu.

Tafakari; tuchukulie kuwa kijana amehitimu kutoka chuo kuu na ana shahada, yaani, anamiliki ujuzi wa kutosha katika nyanja fulani. Akatafuta kazi na mara ghafla mtu akajitokeza na kumwambia: "**Uteuzi wa kazi yako niko nao mimi! Hebu nifuate!**" kisha akamchukua katika uwanja mkubwa, kwenye taasisi kubwa. Na hatimaye akajipata kuwa ndani ya taasisi. Hakuna mtu yeyote aliyemuarifu: "**Taasisi hii ni gani? Ni ya nani? Ujuzi wake ni nini? Inafanya kazi gani?**" hakuna hata mmoja aliyemueleza: "**Uhusiano wako na waajiriwa hawa ni upi? Je wewe ni kiongozi au unaongozwa? Au viongozi na wanaoongozwa ni kina nani?**" hakuna aliye mueleza: "**Kazi yako katika taasisi hii ni kadha wa kadha**". Je, ataweza kutekeleza hatua ya uzalishaji katika taasisi hii? Au je hatua au kitendo chochote atakacho kifanya kitaleta natija? Bila shaka kitaambulia patupu… ((Je, anaye kwenda akisinukia juu ya uso wake ni muongofu zaidi au yule anaye kwenda sawasawa katika njia iliyo nyooka?)) [Al-Mulk: 22]

Mtu aliye sinukia uso wake… macho yake yamefinikwa… hajui njia gani kufuata… kwake yeye na wengine. Ama kwa yule anaye tembea akiwa wima katika njia iliyo nyooka, na macho yanamng'aria juu ya lile analolifanya, huyu basi ndiye yule anayeleta mafanikio kwake na wengine. Amewekwa katika taasisi hii, na hakuna yeyote aliye muarifu taasisi hii inafanya nini… anatakikana afanye kazi gani? Kwa hakika haiwezekani. Kwanza anahitaji kuelezwa: "**Hii ndio taasisi yako. Inafanya kazi hii. Inazalisha hiki. Inapanga hili. Wewe utatekeleza jukumu maalum. Na kazi yako ndani yake… ni hii maalum. Afisi yako itakuwa hapa. Anayehusika na wewe ni mkurugenzi fulani. Wafanyi kazi hawa wako chini ya maagizo yako. Na vifaa na vyombo hivi viko chini ya matumizi yako. Kinacho takikana kwako ni kuzalisha kadha na kadha.** Kufikia hapa ndipo anaweza kuifahamu kazi yake. Ataiimarisha na kutekeleza kile alichoagizwa. Kazi yake itakamilika pamoja na wafanyi kazi wenzake na taasisi yote. Kwa hivyo yeyote anayeifahamu kazi yake kutokana na kile kilicho amuliwa kwake, ndipo juhudi zake za kusifika zitaleta mafanikio katika taasisi hii. Na itazalisha lengo ambalo kwalo taasisi hii imebuniwa.

Lakini, ikiwa yeyote ataachwa ajiamulie na afanye kazi kwa matakwa yake hii haitakuwa taasisi bali badala yake itakuwa uharibifu. Ulimwengu huu ni mfano mkubwa zaidi kuliko mfano huo tulioutaja. Ulihitimu katika ulimwengu baada ya kufika umri wa kubaleghe, na uwezo wako wa kufikiri ukakamilika, umepata shahada ya kuwa na akili timamu, na kuwa mbebaji masuuliya. Katika hatua hii, haitakuwa sawa kwako kuendelea na maisha yako pasi na kutambua maana ya kuwepo kwako katika dunia hii. Si sawa kwako kubebwa kiholela na

*Endelea Uk..9*

watu. Jifahamishe maana ya kuwepo kwako hapa duniani. Hili haliachiwi hekima na busara, kila mwanadamu kuchagua kulingana na matakwa yake, maana ya kuwepo kwake hapa duniani.

Ni yule aliye kuingiza katika taasisi hii… kama tulivyosema awali… mmiliki wa taasisi… yule aliyetoa ruhusa ya kuwepo kwako ndani yake… ndiye aliye fafanua lengo la taasisi hii na ni yeye aliye fafanua jukumu lako ndani yake. Kwa hivyo imekuwa yakini kwako kuwa wewe ni kiumbe cha Allah, na kwamba Yeye ni muumba wa ulimwengu huu, mwanadamu, na uhai, na kwamba alikuleta ndani yake.
((Aliye kuumbeni kutokana na nafsi moja, na akamuumba mkewe kutoka nafsi ile ile. Na akaeneza kutokana na wawili hao wanaume na wanawake wengi…)) [An-Nisaa: 4]

Hivyo basi, wewe ni mmoja wa wale walioenezwa na Allah (swt) ndani ya ulimwengu huu. Yeye ndiye aliye kueneza wewe, na wengine wote katika ulimwengu huu na kukutia katika taasisi hii. Yeye ndiye mwenye kufafanua lengo la kuwepo kwako ndani yake. Yeye (swt) ndiye aliyesema: ((Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi.)) [Al-Mulk: 2]. Kwa hivyo, ni lazima ujue kuwa Allah ndiye aliye kuumba, na wote wanao kuzunguka, ili kukujaribu. Na majaribio haya hupelekea yafuatayo: "Kuishi kulingana na maamrisho na makatazo ya Allah, na wala si kuzama ndani yake au kujitenga nayo; bali kuichukua dunia kama inavyostahili kuchukuliwa. Kwa maana nyengine: Kushibisha nafsiya yako, mahitaji na hisia zako alizokupa Allah kulingana na nidhamu aliyoitunga Allah (swt).

Hapo ndipo utakuwa umepata maana ya kuwepo kwako na utakuwa umetambua jukumu lako katika maisha haya. Allah amekuletea sheria ya uislamu, inayo kuwajibisha ibada, kukuekea sheria za maingiliano, akhlaqi na suluki na kuiwekea jamii sheria za utawala, uchumi, elimu na mahusiano ya kimataifa. Alipoweka sheria zote hizi, alifanya hivyo kuweka nidhamu katika taasisi aliyoiumba na akafanya jukumu lako ndani yake ni kumuabudu Yeye (swt): ((Nami sikuwaumba majini na watu isipokuwa waniabudu mimi)) [Adh-Dhariyaat: 56]. Na ibada hapa sio tu matambiko na vitendo vya kiroho; bali kuabudu humaanisha kupanga mambo yako yote, kulingana na maamrisho na makatazo ya Allah. Hivyo basi, mwanadamu anapotambua maana ya maisha, lengo lake na jukumu lake ndani yake; hapo ndipo atakuwa kweli ameikumbatia imani yake kisawa sawa, hii ni kupitia kufikiri na kuamua na wala si kupitia kuiga au kurithi.

Kufikia nukta hii, imani yake itakuwa ndio msingi wa kufikiri kwake na suluki zake, kwa sababu anajua fika kuwa Allah (swt) anamjaribu na kwamba ulimwengu huu haukuumbwa kwa ajili ya wenyewe tu bali kwa ajili ya yatakayo kuja baada yake. Na Allah amefupisha haya katika aya chache: ((Na ukikufikieni uongofu kutoka kwangu basi atakaye ufuata uongofu wangu, hatapotea wala hatataabika)) [Taha: 123]. ((Na atakaye jiepusha na utajo wangu, basi kwa yakini atapata maisha ya dhiki, na siku ya kiyama tutamfufua hali ya kuwa ni kipofu)) [Taha: 124]. ((Atasema: 'Mola wangu mbona umenifufua kipofu, nami nilikuwa nikiona?)) [Taha: 125]. Atauliza: "**Kwa nini nilikuwa nikiona duniani na siku ya kufufuliwa, siku ya kukusanywa, ni kipofu?**" Allah amemkumbusha kuwa amesahau fungamano la maisha haya na Muumba wake. ((…Mola wangu mbona umenifufua kipofu, nami nilikuwa nikiona?)) [Taha: 125] ((Allah atasema: 'ndivyo vivyo hivyo. zilikufikia ishara zetu, nawe ukazisahau; na kadhalika leo unasahauliwa.)) [Taha: 126]

Mtazamo huu wa maisha, wa yale yaliyokuja kabla yake na yale yatakayo kuja baada yake, na uhusiano wake na kabla yake na baada yake, ndio unaomfanya muumini awe imara katika suluki zake akijifunga na wajibu alioamrishwa na Allah, akijiepusha na aliyokataza Allah. Anafanya kazi katika maisha haya kwa ajili ya kuliinua neno la Allah juu na kulidunisha neno la ukafiri. Na hili ndilo Allah alilolifupisha katika moja ya surah ndogo za Quran ambapo baadhi ya maswahaba na wanazuoni wamesema: "Lau kama hakungeteremka chengine katika Quran, hii ingetosheleza." ((Naapa kwa alasiri!* Hakika mwanadamu bila shaka yuko katika hasara* Ila wale walioamini, na wakatenda mema, wakausiana haki, na wakausiana kusubri)) [Al-Asr: 1-3]

Nasema (neno langu hili) na najiombea msamaha mimi na nyinyi.

((Je! Mwenye kuweka msingi wa jengo lake juu ya kumcha Allah na radhi zake ni bora au mwenye kuweka msingi wa jengo lake juu ya ukingo wa shimo linalo burungunyika, likaburungunyika naye katika moto wa jahanam? Na Allah hawaongoi watu madhalimu)) [At-Tawba: 109].

**Sheikh Ahmad Qasas**
**(Imepatikana kutoka kwa video ya khutba/muhadhara wake)**

# 'MAMA' WASIYEWAHI KUWA NAYE...




Ni mara ngapi macho hayo makali yametilia shaka hadhi yake? Na ni mara ngapi, wanawake hawa walio kiguu na njia masaa ishirini na nne kwa wiki, juhudi zao zimedunishwa kwa kuwa tu 'mke nyumbani'?

Je, hali ni nzuri zaidi kwa kina mama wanaofanya kazi?

Si kweli! Wanavumilia mzigo wa matarajio yasiokuwa ya kihakika – wote walio ndani ya nyumba na nje. Pamoja na msururu wa tuhuma, wanaonekana kama 'washukiwa' katika jukumu lao la mama na mke!

Kina mama wanaofanya kazi dhidi ya mke nyumbani – hakuna la kusitisha mdahalo huu katika upande wa kuvunjika kwa kasi muundo wa kijamii na kifamilia. Hakuna chochote kizuri au kibaya kinachohusishwa na hadhi ya kina mama – iwe wanafanya kazi au la. Hawapaswi kuhukumiwa kupitia fikra iliyojifunga iliyopo katika jamii yetu, ambapo kila Tom, Dick na Harry (yaani watu jumla) wanawabandika majina kulingana na hawaa na matakwa yao.

Lakini, kabla ya kufikia hatma ya kisawa, twahitaji kufahamu maudhui haya katika hali yake ya kihakika.

Si muafaka kujadili juu ya je anastahili kwenda kufanya kazi au la. Tatizo haliko katika kufanya au kutofanya – lipo katika kukiuka kwake mipaka ya kimajukumu kwa mwengine. Tatizo huja wanawake wanapo bwagwa jukumu lao msingi walilotengewa – la mke na mama – kwa ajili ya kutafuta maisha ya kimada yasiyokuwa ya kawaida pamoja na uhuru wa kifedha; maneno haya yanaweza kusikika kama ya kuvutia masikio, lakini nyuma ya kioo upo ukweli mzito unao chukiza…

Natija zake ziko wazi kwetu sisi kuziona na kujifunza kutokana nazo. Kuvunjika kwa familia, watoto wakaidi, ukosefu wa furaha na kutoridhika zimetanda.

Zamani, wanawake hawaku changanyikiwa kuhusu jukumu lao, wawe wanafanya kazi au la. Alitambua kuwa jukumu lake msingi ni kuchunga familia yake, mumewe na kulea watoto wake. Kwa masikitiko kwa kutokea kwa mapinduzi ya kiviwanda, ufahamu huu ukabadilika baada ya vita vya kwanza vya dunia, ambapo mfumo huu wa kimaslahi wa kirasilimali uliwatoa wanawake majumbani mwao, ukawafanya watumwa kifikra kupitia kuwapa 'uhuru', na kuwasukuma katika ajira ili nao wachangie uzalishaji.

Kwa sasa, wanawake wako nje kuinufaisha serikali. Serikali iko juu katika kiwango cha uzalishaji (GDP), wanawake wanatengeza pesa ambazo hawakuwa nazo mwanzoni, pato la mume na mke limeinua kiwango cha maisha kuwa juu wakati wote, huku jukumu la mama likipotea machoni.

Kuna msemo wa kale usemao: "ukimuelimisha mwanamke, umeelimisha kizazi kizima… kwa hivyo, sasa wanawake wameelimika sana, wamefuzu na wamekombolewa pia, ilistahili basi wakilee kwa muangaza kizazi chote… lakini ukweli unasaliti hili. Vijana wa leo wana habari tofauti ya kuhadithia iliozingirwa na mtandao wa majanga ya kutojitambua, upweke, kuchanganyikiwa, madawa ya kulevya, mahusiano yasio halali, msongo wa mawazo, kujiuwa, matatizo ya kiakhlaqi, uhalifu, wizi nk.

Je, ni kitu gani kilichokoseka?

Kuna nukuu moja nzuri iliyowahi kusemwa na swahaba mmoja, walipokuwa katika msafara wa kivita kwenda kueneza ujumbe wa kiislamu, "*Nimekuja kuwakomboa kutoka katika kumuabudu mja kwenda katika kumuabudu muumba wa mja*"

Hapa ndipo tatizo lililopo: maneno haya ni ukumbusho kamili wa hali ya wanawake leo ambapo wamewaruhusu waja kama wao kuwatia thamani yao – mafanikio yao na kufeli kwao. Wanaume wamewakalia juu yao, huku wakiwatawala kama bwana wao. Wamewaruhusu wanaume hawa kuwaendesha – hisia zao, miili yao, fikra zao, nafsiya zao, matakwa yao, na hawaa zao.

*Endelea Uk..11*

Tangu lini wanaume hawa wachafu, wanaoendesha serikali wamekuwa kigezo chetu? Tangu lini wamekuwa ndio wanaotufafanulia sera zetu? Tangu lini wamekuwa ndio watunzi wetu wa kanuni? Tangu lini jinsia ya kike imekuwa dhaifu kwetu? Tangu lini kuwa kwetu kina mama kikamilifu imetudunisha?

Badala ya kumuacha Mola wetu, Allah (swt) kutufafanulia mambo yetu, wanawake wakaanza kujipima thamani yao kwa kujilinganisha na wanaume, kwa kuitikia mwito wa kile serikali inacholingania, na kile vyombo vya habari vinavyosema. Wakadhani kuwa ili kufikia kilele, ni lazima awe kama mwanamume, apate pato kama la mwanamume, avae kama mwanamume, na adhibiti hisia kama mwanamume. Hapo ndipo akaanza kufuata vitu kwa upofu: ikiwa mwanamume aweza kufanya, yeye pia aweza kufanya; huu ndio wimbo. Akaanza kujifakhiri kwa kuitwa dume-jike! Kimakusudi au kwa kutokusudia, hisia hii ikaanza kumzunguka, ya kwamba kile walicho nacho wanaume ndicho kizuri zaidi – kizuri zaidi kuliko kuta nne za nyumba yake na watoto wake.

Allah (swt) amempa mwanamke fadhila ya kipekee ya kuwa mama… kwa nini jambo hili sio tena chimbuko la fahari yetu?
Mtume (saw) atwambia:«الجنة تحت أقدام الأمهات»“Pepo iko chini ya miguu ya kina mama.”

**فقال: يا رسول الله من e جاء رجل إلى رسول الله أحق الناس بحسن صحابتي؟ قال: »أمك« قال: ثم من؟ قال: »أمك« قال: ثم من؟ قال: »أمك« قال: ثم من؟ قال: »أبوك« ((متفق عليه)).**

**Alikuja mtu kwa Mtume wa Allah (saw) akamuuliza, 'ni nani miongoni mwa watu anayestahiki usuhuba mzuri kwangu?' Mtume (saw) akasema: "mamako", akauliza tena, 'kisha nani?' Mtume (saw) akajibu: "mamako", akauliza tena, 'kisha nani?' Mtume (saw) akajibu: "mamako", akauliza tena, 'kisha nani?' Mtume (saw) akajibu: "babako" (Bukhari na Muslim)**

Ukweli wa mambo ni kuwa tumesahau kile Allah (swt) alichotupa ndio bora kwetu. Jamii imetutaka tutoke majumbani mwetu, kuwaacha watoto wetu, tukae ndani ya ofisi tuwe mashini za kutengeza pesa. Na sisi wanawake, pasi na majuto yoyote, tukapiga makamama. Tumekubali ghururi ya jamii – uhuru wa kifedha juu zaidi kuliko kulea watoto wetu, ambapo kwalo kizazi cha binadamu hubakia hai.

Ni kitu gani wanawake hawa walichopata hatimaye?

Watoto wakustaajabisha, kuvunjika kwa nyumba, na kufilisika kinafsi na kihisia. Ufukara wa nafsi zao uko katika aina tofauti tofauti – la muhimu zaidi ni katika malezi ya watoto, ambalo kwalo kizazi cha binadamu hubakia hai.

Hii ndio sababu, twaona msururu wa matatizo miongoni mwa watoto – ni vipi mtoto ataweza kumpenda mamake, wakati hajawahi kuwa naye? Wanalolijua ni jina pekee!

Wazazi leo wanalalamika kutelekezwa umri wa uzeeni, je hawakumbuki namna walivyo athiri pia hamu ya mtoto kwao katika miaka ya utotoni mwake yaani kukosa makini. Jinsi gani alivyo pigana na upweke wakati wao wakitengeza pesa…

Je chekechea au mayaya, wanaweza kuchukua nafasi adhimu ya mama kwa mtoto wake? Natija yake, hili huathiri ukuaji wa mtoto kihisia na kijamii. Tabia isiyokuwa salama na ya kihuni ya mfanyikazi humuathiri mtoto kisaikolojia.

Twahitaji kutafakari tena upya – ni nani anayetufafanulia majukumu na masuuliya yetu msingi, ni yule aliye tuumba, au miondoko iliyobuniwa na watu wasiofikiri ili kutimiza ulafi wao?

Twahitaji kufahamu, watungaji sera hawa wa kirasilimali, wanawatumia wanawake, kwa maslahi yao wenyewe. Hawako kuwajali wanawake bali kujali faida. Kama kweli wanazingatia kuhusu kupewa uwezo mwanamke, mbona basi hutuoni msururu wa maraisi wanawake?

Kumbuka, ni Allah, ndiye aliye tukirimu kwa ule uhalisia wetu kuwa kina mama, waliotukuzwa zaidi.

Mwanamke mmoja alimwambia Mtume (saw), 'Ewe Mtume wa Allah, umewapa bishara wanaume na sio wanawake'. Mtume (saw) akasema,

**أفما ترضى إحداكن أنها إذا كانت حاملا من زوجها» وهو عنها راض أن لها مثل أجر الصائم القائم في سبيل الله، فإذا أصابها الطلق لم يعلم أهل السماء وأهل الأرض ما أخفي لها من قرة أعين، فإذا وضعت لم يخرج منها جرعة من لبنها، ولم يمص مصة، إلا كان لها بكل جرعة وبكل مصة حسنة، فإن أسهرها ليلة كان لها مثل أجر سبعين رقبة تعتقهن في سبيل الله«**

“Je haridhiki mmoja wenu kwamba anapokuwa na uja uzito wa mumewe na huku yuko radhi na yeye ana ujira mfano wa aliye funga na aliye simama katika njia ya Allah, anapopatwa na uchungu wa uzazi watu wa mbinguni na ardhini hawajui kilichofichika tumboni mwake kinachomfurahisha yeye machoni. Na anapojifungua hakuna tone la maziwa linatoka na hakuna tone la maziwa mtoto analo nyonya isipokuwa atapa ujira wa jema moja. Na mtoto anapomkesheza usiku atapata ujira mfano wa aliye waacha watumwa sabiini huru kwa ajili ya Allah" [Tabarani]

Kulingana na uislamu, jukumu msingi la mwanamke ni mama na mjengaji nyumba kwa sababu ni kupitia kitendo hichi ndipo kizazi husimamishwa…

**"Kina mama hucheza dori kubwa katika kuunda kizazi. Kila mama anavyo kuwa mzuri katika kulea watoto wake, ndivyo umma unavyo faulu kuundwa na unavyofaulu kuzalisha mashujaa. Ni nadra kuona mwanamume imara isipokuwa nyuma yake kuna mwanamke imara aliye acha suluki zake ndani ya shakhsiya yake kwa njia ya maziwa ambayo kwayo alinyonyeshwa na harara ya kikumbatiwa kila alipohitaji hifadhi." Sheikh Abdullah Azzam (Rahimahullah).**

Ni muhimu sana kwa wanawake leo kuunganisha vitendo vyao na hukmu za kisheria kujilinda na fitna za nje. Tusiwalee watoto wetu kwa kuwa tu

*Endelea Uk..12*

ni ada iliyowekwa katika jamii, hivi ndivyo wanawake walivyokuwa wakifanya kwa makarne, bali ni kutambua kuwa ni jukumu ambalo Allah (swt) ametupa sisi, ambalo tutahesabiwa, na kwa amali zetu ndogo, tutalipwa na Allah (swt). Na hii ni ibadah kwetu.

Sio waislamu pekee, hata wasiokuwa waislamu wanajua umuhimu wa wanawake kukaa majumbani na kulea watoto wao. Mmoja katika mjumbe wa bunge la congress la Amerika alisema kuwa, 'Kwa kuwa Allah amempa uwezo wa kuzaa, hawapaswi kuwaacha na kwenda kufanya kazi. Ni nani atakaye kaa nyumbani kuwachunga?'

Samuel Smilles, muanzilishi wa tafakari ya uzazi upya (renaissance thinking), alisema pindi serikali zilipoanza kuwaajiri wanawake, licha ya mchango wao kwa utajiri wa taifa, ilisababisha matokeo ya kuumiza kila ongezeko na tegemeo la wanawake katika nguvu kazi lilivyozidi. Ilishambulia muundo wa maisha ya nyumba, ikawapokonya watoto mama zao, waume wake zao, na watoto jamaa zao, iliwapokonya wanawake haki yao na majukumu yao kwa familia zao.

Mwanafalsafa wa kiuchumi, Jules Simon alisema katika majarida ya journal v. 17, wanawake wameingizwa katika kila sekta kuanzia mitambo ya ushonaji mpaka katika taasisi za benki ilhali wengi wa wanawake hawa walikuwa na uwezo mkubwa juu ya waajiri wao lakini wakalipwa pauni chache. Mume sasa akawa amepata faida ya kimada kwa kuwa na mke anayepata mshahara; huku wakati huo huo mke ikitishia kuchukua nafasi yake katika nguvu kazi. Pili alitaja kuwa waajiri wamewavua wanawake majumba yao na familia zao.

Daktari Ida Ellen adai katika matokeo ya utafiti wake kuwa kuna uhusiano mkubwa baina ya idadi ya wanawake wanaofanya kazi na kiwango kikubwa cha uhalifu katika jamii hiyo. Alihitimisha kwa kusema kuwa mzizi wa mgogoro wa kifamilia Amerika na kiwango kikubwa cha uhalifu katika jamii ni kutokana na mwanamke kuacha nyumba yake kwenda kuongeza mara dufu kiwango cha pato la familia. Huku kiwango cha pato kikiongezeka ndivyo kiwango cha maadili kilivyo pungua. Daktari Ellen alitoa wito wa kurudi kwa mwanamke nyumbani kwake kurekebisha jamii na maadili yake, kuwa ndio njia pekee ya kukiokoa kizazi kipya kutokana na muozo.

Bwana Byron, malenga wa kiingereza, adai kuwa wanawake wanapaswa kuhudumia nyumba zao na kuwafundisha dini watoto huku akitahadharisha juu ya matangamano huru baina ya wanawake na wanaume.

Chimbuko la muongozo wetu daima liwe ni Quran na Sunnah, na wala si kile kinachosemwa na jamii. Hebu tusimameni, tujitose, na tusimamishe kizazi chenye shakhsiya za kiislamu, tuwaelimishe watoto wetu kumpenda Allah (swt), kufuata kitabu chake kabla hatujachelewa. Chaguo ni letu pekee, ikiwa twataka starehe za muda za dunia, au pepo ya milele chini ya miguu yetu.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

**Nilofar Shamsi**

# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

## Halaqa 2: Nukta ya Kusomesha na Kujenga Thaqafa

Tulisema hapo Awali kuwa Da'wah ya Mtume صلى الله عليه وسلم imegawanyika katika nukta (marhala) tatu. Kuhusu nukta (Marhala) ya kwanza imejumuisha kusomesha na kujenga thaqafa kwa ajili ya kufikia shabaha mbili nazo ni:

1. Kujenga Shakhsiya ya Kiislamu
2. Kuandaa kundi (chama) litakalobeba Da'wah

Makkah ikawa ndio nukta kianzio ambayo ilipatikana kwayo Halaqa ya kwanza Mtume (saw) akafanya kazi nao kuleta mageuzi. Alianza Mtume (saw) Da'wah yake kwa Jamaa zake wa karibu na watu wake wa nyumbani kisha kwa Qawmu yake. Wakasilimu waliosilimu, kisha akawa anawapa Thaqafa waumini. Na kuwasomesha kilichoteremka katika Qur'an, akiwa mbali na macho ya mushrikina.

Mtume (saw) alikuwa akikutana na maswahaba zake (ra) kwa siri katika nyumba ya Arqam Ibnu Abi Arqam (ra) au wakati mwingine katika mapango ya Makkah usiku wa kiza ama mchana wakati wa jua kali. Akawa katika Thaqafa anayowapa anachunga mambo mawili msingi:

**Kwanza:** Kujenga Aqeedah (Itikadi) ya Uislamu katika nafsi zao; ili wapate ufahamu wa ndani katika kuifahamu na kuimakinisha ndani ya nafsi zao misingi ya Aqeedah (Itikadi) ya Uislamu, ili asiweze yoyote kuing'oa.

**Pili:** Kujenga katika maswahaba zake (ra) Shaksiyyah (Muonekano) ya Kiislamu na kumakinisha ndani yao Aqliyyah na Nafsiyyah ya Kiislamu ili mfumo wa Kiislamu uwe ndio mwili wao, wawe ni majeshi ya Allah (swt) wanaotii Amri zake, wanao wabebea watu risala ya uongofu na nuru ya Uislamu. Hatimaye waweze kuwa na uwezo wa kuwafahamisha na kuwakinaisha wengine. Maanake wao watakua wabebaji Da'wah na ndio wanao uongoza Ummah. Kwa sababu hiyo walihitajika sana wawe ufahamu wa ndani na uweza wa kuwalingania watu kwa dini ya Allah (swt).

Mtume (saw) hakuficha Da'wah japo alificha muundo wa kundi/chama kwani alikua akilingania kwa dini ya Allah (swt) mchana wazi wazi na huku akiwasomea watu wake:

يأيها الناس إني رسول الله إليكم جميعا)

"Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume kwenu nyinyi nyote, niliye tumwa na Mwenyezi Mungu Mwenye Ufalme wa mbingu na ardhi. Hapana mungu ila Yeye anaye huisha na anye fisha. Basi muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake asiyejua kusoma na kuandika, ambaye anamuamini Mwenyezi Mungu na maneno yake. Na mfuateni yeye ili mpate kuongoka"
[Al-A'raaf: 158]

Aliendelea na Da'wah yake tokea siku ya Kwanza kama alivyopokea Bukhari kutoka kwa Ibn Abbas (ra) asema; ilipoteremka:

وأنذر عشيرتك الأقربين

"Na uwaonye jamaa zako walio karibu nawe"
[Ash-Shu'araa: 214]
Mtume (saw) alipanda juu ya Swafaa na akawa anaita: "Enyi Baniy Fihri! Enyi Baniy Adiyyi!" mpaka wakakusanyika Maqureysh wakijumuisha Abu Lahab, hata mtu ambaye hakuweza kutoka alituma mjumbe akatizame kuna nini. Kisha Mtume (saw) akawaambia: "Je mwaonaje lau nitawaambia kua nyuma ya hili jabali kuna maadui wamekuja kuwapiga vita, Na wanataka kuwashambulia mtakua ni wenye kunisadikisha? Wakasema: Ndio, hatujapatapo uongo kutoka kwako! Mtume (saw) akaendelea kuwaambia: Basi mimi bi muonyaji kwenu kwa adhabu kali. Akasema Abu Lahab: Maangamivu yakushukie mchana wote huu! Kwa sababu hii ndio umetukusanya hapa? Ikateremka:

تبت يدا أبي لهب وتب

"Imeangamia mikono ya Abu Lahab, na na yeye pia ameangamia."
[Al-Masad: 1]

Mtume (saw) akafanya Makkah ndio sehemu kianzilio kwani hakutoka katika nukta (marhala) ya kwanza ambayo iliendelea kwa muda wa miaka mitatu (3). Hatimaye Allah (swt) akamuamrisha kudhihirisha Kundi (Chama) lake na harakati yake kumwambia:

فاصدع بما تؤمر واعرض عن المشركين انا كفيناك المستهزئين الذين يجعلون مع الله الها آخر فسوف يعلمون

"Basi wewe yatangaze uliyoamrishwa, na jitenge na washirikina"
[Al-Hijr: 94]

Kwa maana Mtume (saw) alitoka wazi kwa kudhihirisha Amri ya Mola wake wala hakujali wanayoyasema mushrikina akiwa na hakika Mola wake atamkinga na shari za maadui zake na wanaomcheza shere. Kwa kauli hiyo akatoka Mtume (saw) na maswahaba zake (ra) wakiwa katika safu mbili wakielekea Ka'bah kwa mpangilio ufuatao:

**Safu ya Kwanza** ikiongozwa na Hamzah bin Abdul Mutwalib (ra) na **Safu ya Pili** ikiongozwa na Umar ibn Khatwab (ra).

Wakafika hapo mbele ya macho ya mushrikina na ikawa kitendo cha kutoka wazi kikawa ndio mwanzo wa nukta (marhala) ya pili ambayo ni nukta ya maingiliano (tafaul) na Ummah waziwazi.

**Itaendelea katika UQAB Toleo 7… In Shaa Allah.**

# SWALI/ JAWABU: Ni Kipi Kilicho Nyuma ya Mgogoro Baina ya Saudi Arabia na Qatar?



**Swali:**

Trump alisema katika mkutano wa waandishi habari akiwa na mwenzake wa Romania katika ikulu ya White House mnamo 9/6/2017: ((…wahusika wakuu katika eneo wamekubaliana kusitisha ufadhili wa ugaidi, ima kifedha, kijeshi au hata kusaidia kimaadili. Taifa la Qatar, kwa bahati mbaya, kihistoria limekuwa mfadhili mkubwa wa ugaidi. Na kwa kutokea kwa mkutano huo, mataifa yalikuja pamoja na kuongea nami kuhusu kuikabili Qatar juu ya tabia yake. Kwa hivyo tukawa na uamuzi wa kufanya: tuchukuwe barabara sahali, au hatimaye tuchukue kitendo kigumu lakini kinachostahili?

Ni lazima tukomeshe ufadhili wa ugaidi. Nimeamua, pamoja na waziri wa kigeni Rex Tillerson, makamanda wetu wakubwa na wanajeshi, wakati umewadia kutoa wito kwa Qatar kukomesha ufadhili…)) [Al-Youm As-Sabi', 9/6/2017]. Je, hii yamaanisha kuwa mgogoro baina ya Saudi Arabia na Qatar umesukumwa na Trump? Ikiwa hii ni kweli, kwa nini Trump anachukua hatua hii, akitambua kuwa kambi kubwa ya kiamerika katika eneo iko Qatar? Vyombo vya habari pia vimenasibisha msimamo wa Qatar juu ya iran, kundi la Ikhwan, au Hamas, kama sababu ya utesi wa kisiasa baina ya Saudi Arabia na Qatar. Tuelewe vipi taarifa ya Trump kuambatana na yale yanayokorogwa katika vyombo vya habari? Na mgogoro huu waelekea wapi? Je utapelekea kujiondoa au kufukuzwa kwa Qatar kutoka katika jumuia ya ghuba? Shukran.

**Jibu:**

Kwanza: ndio, anayesukuma mgogoro huu uliojitokeza ni Amerika. Kwa maana nyengine, ni raisi wa Amerika Trump, lakini kabla ni fafanue juu ya hilo, naanza na sehemu ya mwisho ya swali. Baadhi wanafikiri kuwa sababu ya mgogoro wa ghuba wa Qatar, kama ulivyo ripotiwa na vyombo vya habari au kama unavyo chochewa, ni usaidizi wa Qatar kwa (kundi la) Ikhwan al-Muslimeen au ushirikiano wake wa kimikakati na Iran, huku wengine wakisema kuwa sababu halisi ya mgogoro huu ni kutokana na utesi wa jadi baina ya familia ya Hamad na familia ya Zayed ulioanza miaka ya sabiini wakati Imarati ilipobuniwa. Hii ilipelekea Saudi Arabia kumfuata mshirika wake, Imarati kushambulia Qatar. Kuna waandishi waliosema kuwa mgogoro huu wa kuitenga Qatar unahusishwa na 'Israel'. Kwa mfano ni nukuu ya CNBC kutoka kwa Jake Novak:

"Kijuu juu, ni sahihi kabisa kusema mfarakano huu wakufurahisha baina ya Saudi Arabia na Qatar ni kuhusiana na Iran kwani wasaudi wamerengwa na jinsi gani ya kupunguza nguvu na athari za Iran katika Masharaki ya Kati zinazo endelea kukua, lakini ukizama ndani kidogo, yanaonekana zaidi ya hayo, nayo ni kuwatenga waqatari katika wakati huu maalum kuna uhusiano na nchi

Endelea Uk..15



Email: uqab@hizb.or.ke

nyengine: Israel" (Arabi 21, 7/6/2017)

Lakini kwa kufikiria na kudadisi kwa undani kila kitu kilichotokea, hukana mambo haya; si mageni, na Qatar imekuwa ikiyafanya kwa muda mrefu, wala hayakufanywa upya hivi sasa. Ukuruba wa Qatar kwa Iran unajulikana na uhusiano wake na Hamas ni maarufu pia. Zaidi ya hayo, athari ya mahusiano kati ya Qatar na serikali inayokaliwa na mayahudi ya Palestina na mahusiano kati ya nchi hizi na Saudi Arabia na Imarati pia hayakufichika, na hata mahusiano ya kikabila hayafikii kiwango hiki cha hali ya juu. Mambo haya yote yalikuweko kabla ya mgogoro na yatakuweko hata baada ya mgogoro; kwa hivyo, sizo sababu halisi.

Pili: sababu halisi, kama nilivyotangulia kutaja mwanzoni, ni Amerika au Trump na kutambua hili, tunarudia mambo yafuatayo:

1 – Tangu mwanzoni mwa karne hii, Qatar imekuwa "jiko" kuu la siasa za kiingereza katika eneo hili. Al-Jazeera imekuwa jukwaa kuu la habari kukatiza siasa ya Amerika na kushambulia vibaraka wa Amerika katika eneo hili. Jambo jengine ni pesa za kisiasa ambazo zimekuwa smaku kubwa ya kisiasa kuvutia nguvu za kisiasa. Kupitia vifaa hivi viwili, Qatar imepata mafanikio makubwa hususan katika harakati za kiislamu zinazotambuliwa kama za 'kati na kati' nchini Palestina, Misri, Libya, Tunisia na kwengineko, na Doha nchini Qatar imekuwa pepo ya viongozi wa harakati hizi na kitovu cha kupanga na kuharibu siasa na vibaraka wa Amerika. Na kama ilivyo tabia ya Uingereza kujifanya iko pamoja na Amerika huku ikitaka kuiharibia mambo yake, Qatar imeuelewa vyema mchezo wa Uingereza, na tangu 1991, iliikaribisha kambi ya kiamerika ya Al Udeib ambayo ndio makao makuu ya kitovu cha utoaji amri za kijeshi la Amerika (American Central Command) na ni kambi muhimu ya angani ambayo kwayo ndege za kiamerika hurukia kwenda kueneza mauaji na uharibifu miongoni mwa Waislamu Iraq, Afghanistan, Syria na Yemen. Huu ulikuwa wakati ambao Uingereza ilikuwa ikijenga "jiko" lake la kisiasa nchini Qatar mpaka lilipo malizika na kujitokeza katika mwanzo wa karne hii.

Kisha, jukumu la Qatar, kama mtumwa wa Uingereza, lilikuwa kwa ulaini kuambatana na mpango uliochorwa. Amerika ilikerwa na jukumu hili la Qatar kufikia nukta ya hasira zilizompelekea George W. Bush, mwana, kukadiria kukipiga bomu kituo cha Al-Jazeera kulingana na habari zilizo chapishwa na DW mnamo 22/11/2005:

(Gazeti la kiingereza "The Daily Mirror" mnamo Jumanne lilinukuu waraka wa 'siri ya juu' kwa afisi ya waziri mkuu wa Uingereza kutoka kwa raisi George W. Bush kwamba mnamo 2004 alifikiria kuyapiga bomu makao makuu ya kituo cha runinga ya setlaiti cha 'Al-Jazeera' nchini Qatar) (DW 22/11/2005). Huu ndio umekuwa msimamo wa eneo la Ghuba mpaka alipoingia mamlakani mfalme Salma wa Saudi Arabia.

Saudi Arabia imesimama na Amerika, na tangu hapo idara ya Obama iliamua kumuamini kibaraka wake Salman na jukumu muhimu katika eneo, nalo ni, upande mmoja, kuhitilafiana na jukumu la Qatar na kulitawala, na upande mwengine, kuambatana na mipango mipya ya kiamerika. Kwa hivyo, imelipa nguvu jukumu la vibaraka wa Amerika na imeuchukuwa utesi kati ya Saudi Arabia na Qatar kufikia hatua inayo hatarisha jukumu lote la Qatar. Na baada ya kuingia madarakani raisi mpya wa Amerika Donald Trump mapema mwaka huu, siasa ya Amerika imekuwa kali zaidi na isiyo pinda katika kukabiliana na kadhia nyingi za kimataifa, ikiwemo Qatar.

2 – Wakati wa ziara ya Trump jijini Riyadh mnamo 20-21/5/2017, aliwakusanya pambizoni mwake viongozi 50 Salman akiwa ubavuni mwake. Kwa kugusia ufadhili wa Qatar kwa ugaidi, Qatar ilitambua kupitia wadaku wa Kiingereza kuwa Amerika imeanza hatua kali za kulinyanyua jukumu la Saudi na kuvuruga jumuku la Qatar na Uingereza katika eneo la ghuba. Kujibu hatua hii, taarifa za Qatar zilitolewa siku mbili baada ya Amiri wa Qatar kurudi kutoka Riyadh.

Shirika la habari la Qatar lilinukuu taarifa za Amiri wa Qatar, Tamim Al-Thani, mnamo 23/5/2017: "Kile kinacho ianika Qatar kutokana na kampeni dhalimu ikisadifiana na ziara ya raisi wa Amerika katika eneo, inayo lenga kuihusisha (Qatar) na ugaidi… Tunashutumu tuhuma za kufadhili ugaidi… hakuna mtu yeyote aliye na haki ya kututuhumu ugaidi kwa sababu wame iorodhesha Ikhwan al-Muslimeen kama kundi la kigaidi.

Alitoa wito kwa Misri, Imarati na Bahrain kurudia upya msimamo wao dhidi ya Qatar… Kuna uhusiano imara na Amerika licha ya mambo yasiyo kuwa mazuri yalioko kwa sasa ya idara ya Amerika tukiwa na imani kuwa hali hii haitaendelea kwa sababu ya uchunguzi wa mahakama dhidi ya dosari na ukiukaji mipaka wa raisi wa Amerika, na kambi ya Al Ubeid inawakilisha himaya kwa Qatar kutokana na matarajio ya nchi jirani, lakini ndio fursa pekee ya Amerika kumiliki athari ya kijeshi katika eneo, na Qatar haijui ugaidi wala msimamo mikali, na ingependa kuchangia kupatikana uadilifu na amani kati ya Hamas, muwakilishi halali wa wapalestina, na Israel, kwa kuendeleza mawasiliano na pande zote.

Qatar imefaulu kujenga mahusiano imara kwa Amerika na Iran wakati huo huo kwa sababu Iran inawakilisha athari ya kieneo na ya kiislamu ambayo haipaswi kudharauliwa na si busara kuyakuuza mambo kwayo (athari). Taarifa hizi zaashiria kuwa Qatar inamtuhumu Trump kuwa nyuma ya kampeni dhidi ya Qatar ya kuituhumu kufadhili na kuunga mkono ugaidi. Taarifa hizi zilikuja pindi baada ya kongamano la Trump pamoja na wawakilishi wa serikali zilizoko katika ulimwengu wa kiislamu ambapo Trump alikuwa makini kuonyesha mafanikio yake katika kuziongoza serikali hizi kufikia malengo ya Amerika na utiifu kwa Amerika. Trump alisema katika kongamano hili kuwa, baadhi ya nchi, akikusudia Qatar, zinafadhili ugaidi. Kwa hivyo, taarifa

Endelea Uk..16

za Qatar ni sawa na jibu kwa Trump kwa kuwa inataka kumzamisha na kutaraji kuwa atang'atuliwa mamlakani kutokana na uchunguzi wa mahakama dhidi yake.

3 – Mkusanyiko wa wafalme 55, maraisi na viongozi (wa ujinga na uharibifu) wa Ghuba na biladi za kiarabu na kiislamu huko Saudi Arabia, unawakilisha kujitolea kwa Saudi kufuata mpango wa Amerika wa kuonyesha uongozi wa Saudi eneo hili. Hii haikuwa ishara ya kimakosa kutoka Washington inayotaka kuviweka visima vya mafuta katika utumizi wake chini ya kisingizio cha tishio la Iran upande mmoja, na kuuzima moto wa athari ya Uingereza katika nchi za Ghuba kwa kuufanya uongozi wa Saudi ndio wenye kudhihiri na kuzifanya nchi za Ghuba zilizosalia kutembea nyuma ya Saudi Arabia, yaani, nyuma ya siasa ya kiamerika.

Hivyo basi, Saudi Arabia hainge weza kuvumilia wale wanaosimama dhidi ya uongozi wake katika eneo, na macho yake yalikuwa wazi kwa Qatar na ilikuwa inasubiri tu tukio litakalo itia Qatar motoni.

Kwa hivyo, ilikuwa mkali kwa taarifa za Qatar dhidi ya Saudi Arabia na Amerika zilizo chapishwa na shirika la habari la Qatar mnamo 23/5/2017. Licha ya kuomba radhi kwa Qatar, Saudi Arabia haikukubali maelezo ya Qatar, lakini ikaziona taarifa hizi kama thibitisho la kukataa kwa Qatar siasa ya kisaudi na jukumu la Amerika ililompa Salman, ndipo mgogoro ukaanza. Saudi Arabia ilijitoa kimasomaso na kutangaza kukata mahusiano na Qatar, ilionyesha ukali dhidi ya Qatar kwa kusimama dhidi ya uongozi wa Saudi katika Ghuba, huu ni mmuliko wa misimamo imara ya idara ya Trump. Hatua za Saudi Arabia zilikuwa kali dhidi ya Qatar na zilikuwa zimepita mpaka mnamo 05/03/2014 ilipo muondoa balozi wake kutoka Qatar, iliyo onekana kama kuzingirwa kwa Qatar. Kuwa na athari kubwa na kufuata njia ya Amerika, zikaja hatua za kisaudi za kushtua; waqatari walipewa masaa 48 pekee kuondoka nchini humo.

Kwa kukubalina na njia ya ushtuaji ya kiamerika, sambamba na mienendo ya Saudi na kwa kusadifiana nayo, Misri iliirudisha ndege ya abiria ya Qatar na kutoiruhusu kuingia eneo lake pasi na kutoa ilani mwanzoni na ndivyo zilivyo fanya nchi nyenginezo washirika wa Saudi dhidi ya Qatar.

Inaoneka kana kwamba Qatar ilishtuliwa na maamuzi haya ya kuisusia wala haikuyatarajia. Waziri wa kigeni wa Qatar, Mohammed Bin Abdulrahman Al-Thani, alisema katika mahojiano na BBC mnamo 6/6/2017 kuwa "Hatua zilizochukuliwa dhidi ya nchi hii ni za kushtua, na kilichotokea ni "Adhabu ya kijumla ya nchi tatu katika eneo hili ambazo zimejaribu kulazimisha ususiaji wa Qatar na watu wake…"

Qatar haipaswi kuonekana kama kakamavu katika kuikabili Amerika au vibaraka wake, kama Saudi Arabia, isipokuwa kuwe na nchi kubwa inayoisaidia na kusimama nyuma yake kufanya hilo, ambayo bila shaka ni Uingereza, ambayo Qatar inafuata siasa yake kwa siri, bali hata dhahiri! Lengo la Uingereza ni kuiharibia Amerika na kuvuruga mipango yake ya kumakinisha athari yake katika eneo, haswa eneo la Ghuba, na kwa hivyo iliwaagiza vibaraka wake ndani ya Qatar kufanya hivyo. Uingereza haikutarajia matokea yake kuwa ya kushtua kana kwamba ilikuwa inatarajia kuondolewa kwa mabalozi kama mnamo 2014, na mambo yamalizike pasi na natija kubwa, haswa kule kuwa Qatar yatumia kuwepo kwa kambi kubwa ya kiamerika humo kama himaya. Na kwa hivyo ilinukuliwa katika taarifa za Amiri wa Qatar zilizo chapishwa na shirika la habari la Qatar mnamo 23/05/2017, ambapo ilizifuta baadaye na kudai kuwa tovuti yake ilivamiwa: "Kambi ya Al Udeid inawakilisha himaya kwa Qatar kutokana na matarajio ya nchi jirani, lakini ndio fursa pekee ya Amerika kumiliki athari ya kijeshi katika eneo." Hili ndilo Qatar inalotegema kuinyamazisha Amerika, huku ikivuruga na kuingilia dhidi ya Amerika na vibaraka wake katika eneo kupitia kituo chake cha Al Jazeera. Iliipa Amerika kambi kubwa zaidi katika eneo, na hivyo basi ikashangazwa na vitendo hivi vya kikatili.

4 – kwa hivyo, sababu halisi ya mgogoro huu ni jukumu jipya la Salman lililochorwa na Trump; kuwa kiongozi wa eneo la Ghuba, kutabikisha siasa ya Amerika, na kumzuia yeyote katika vibaraka wa Uingereza kuiingilia au kuivuruga, na kwa kuwa Qatar ndio iliochanguliwa na Uingereza kutekeleza jukumu la Uingereza la kuingilia na kuvuruga mipango ya Amerika katika eneo hili na kutabikisha mipango ya Uingereza, hatua ya ukali isiyokuwa ya kawaida ilichukuliwa dhidi ya Qatar. Amerika ndio dereva nyuma ya Salman katika mgogoro huu wala haikuficha hili, lakini ilikuwa ikijifichua pole pole kuwepo nyuma ya yale yaliyotokea na yanayo endelea kutokea:

Mtandao wa Al-Arabiya uliripoti mnamo 6/6/2017 taarifa ya afisa wa ngazi ya juu katika idara ya Amerika kwa shirika la habari la Reuters: "Kiwango kikubwa cha tabia ya Qatar kina ogopesha sio tu majirani zetu wa Ghuba bali Amerika vile vile". Afisa wa ngazi ya juu katika idara ya Amerika aliliambia shirika la habari la Reuters mnamo Jumatatu kuwa Amerika haitaki kuona 'mfarakano wa kudumu' baina ya nchi za Ghuba, baada ya nchi kadhaa za Ghuba na za kiarabu kuamua kukata mahusiano na Qatar mnamo Jumatatu kutokana na madai ya kusaidia makundi yenye misimamo mikali na Iran, afisa huyu aliongeza kusema: "Twataka kuwaleta katika muelekeo wa sawa."

- Shirika la BBC liliripoti mnamo 6/6/2017: (Raisi wa Amerika Donald Trump alidokeza athari ya ziara yake ya Ghuba ya hivi karibuni juu ya uamuzi wa kukata mahusiano na Qatar, na Trump akasema alipokea habari wakati wa ziara yake kuwa Doha inafadhili harakati za "ki mfumo zilizo na misimamo mikali."

"Wakati wa ziara yangu ya hivi karibuni Mashariki ya Kati, nilieleza kwamba kamwe hakuwezi kuwepo tena ufadhili wa mfumo ulio na msimamo mkali. Viongozi wakainyoshea

Endelea Uk..17



Email: uqab@hizb.or.ke

kidole Qatar – tamaza!” akaandika.

“Ni vizuri sana kuiona ziara ya Saudi Arabia huku mfalme wake na nchi 50 tayari zikilipa. Walisema watachukua hatua ngumu dhidi ya ufadhili wa misimamo mikali, na maregeleo yote yalikuwa yanaelekea kwa Qatar. Pengine huu utakuwa ndio mwanzo wa mwisho wa tishio la ugaidi!” baadaye akaendelea.

Taarifa za Trump mnamo 9/6/2017 zinafichua na kuthibitisha kuwa Amerika iko nyuma ya mshawasha wa Saudi:

(Raisi wa Amerika Donald Trump mnamo Ijumaa alisema kuwa Qatar isimamishe kufadhili ugaidi haraka iwezekenavyo na alitaraji kuwa kongamano la Riyadh litakuwa ni mwanzo wa kumalizika kwa ugaidi. “Katika mkutano na waandishi wa habari pamoja na mwenzake wa Romania ikuluni white house alisema, kwamba Qatar kihistoria imekuwa ni nchi inayo fadhili ugaidi.” (Sky News Arabia, 9/6/2017)

Donald Trump alisema: “…wahusika wakuu katika eneo la Ghuba wamekubaliana kusitisha ufadhili wa ugaidi, ima kifedha, kijeshi au hata kimaadili. Taifa la Qatar kwa bahati mbaya, kihistoria limekuwa mfadhili wa ugaidi kwa kiwango kikubwa. Na kwa kutokea kwa kongamano hilo, mataifa yalikuja pamoja na kusema nami kuhusu kuikabili Qatar juu ya tabia yake hii.”

(Kwa hivyo tulikuwa na uamuzi wa kufanya: Je, tufuate barabara sahali au hatimaye tuchukue kitendo kigumu lakini kinachostahili? Lazima tukomeshe ufadhili wa ugaidi. Nimeamua pamoja na waziri wa kigeni Rex Tillerson, magenerali wetu wakuu na wanajeshi, wakati umewadia kutoa wito kwa Qatar to kukomesha ufadhili wake…)(Al-Youm As-Sabi’,9/6/2017)

5 – Ama kuhusu ni wapi mgogoro huu wa Qatar unapo elekea, Qatar imepigwa na butwaa na misimamo hii migumu kutoka kwa vibaraka wa Amerika, Saudi Arabia na Misri ambao vibaraka wa Uingereza kama, Imarati, Bahrain na wengineo, wamefuata katika ile mbinu ya Uingereza ya kugawanya majukumu kama tulivyotaja katika jibu la swali tulilotoa mnamo 9/4/2017 ambapo tulisema: (… Kwa hivyo ni wazi kuwa Uingereza inagawanya majukumu ya vibaraka wake kwa njia inayoonekana kugongana, lakini mwishowe hufikia lengo la Uingereza; haiwaweki vibaraka wote katika upande mmoja, haswa katika nchi ambazo kuna karata kadhaa). Qatar, kama tulivyo sema, haikutarajia mgogoro huu kukua kwa nguvu na ukali. Hatua za Saudi zilishtua; mabalozi wa Qatar walipewa masaa 48 kuondoka nchini mwake. Kwa kukubaliana na mbinu ya kiamerika ya kutia mshtuko na kwenda sambamba na hatua za Saudi, Misri ilizirudisha ndege za abiria za Qatar na ikazikataza kuingia eneo lake kabla ya kuzipa ilani mwanzo, na hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa nchi nyenginezo washirika wa Saudi Arabia dhidi ya Qatar.

6 – Je, hili litapelekea kujiondoa au kufurushwa kwa Qatar katika jumuia ya Ghuba? Inawezekana kama hatua ya mwisho, lakini inatarajiwa sana kuwepo na uwezekano wa kutatua mgogoro huu. Dola mashuhuri za kiulimwengu kama Amerika na Uingereza, zote zina hamu Qatar ibakie katika jumuia ya Ghuba kwa malengo tofauti tofauti ambayo kila mmoja anayataka.

Kwa Amerika, inataka Qatar, kama ilivyotajwa juu, kuwa chini ya uongozi wa Saudi Arabia; yaani, kutekeleza maslahi ya Amerika bila ya kuingilia au kuvuruga kwa sababu tofauti tofauti. Amerika inataka kambi yake iwe imara na kutekeleza majukumu yake bila ya kukatizwa. Inatambua kuwa Uingereza iko nyuma ya Qatar, na kwa kupitia mbinu zake za kijanja, inaweza kuiletea kambi yake matatizo mengi ikiwa Qatar itajiondoa katika jumuia ya Ghuba. Hivyo basi, Amerika inaitaka Qatar kutabikisha mipango yake na kuwa sehemu ya muelekeo wa Saudi na wakati huo huo kubakia katika jumuia ya Qatar.

Uingereza nayo inataka kuibakisha Qatar katika jumuia ya Ghuba kwa sababu, ndani ya jumuia hii, inaweza kufanya kazi nyuma ya pazia yake kutabikisha mipango ya Uingereza kulingana na muelekeo wa Uingereza ambayo ina sura mbili; inaonyesha urafiki upande wa mbele, na kudunga kisu upande wa nyuma. Kwa hivyo, kile kinacho tarajiwa kama tulivyotaja juu ni suluhisho litakalo zunguka katika kuzuia hatima ya kuraruka kati ya Qatar na jumuia ya Ghuba isipokuwa labda hii itokee kama “hatua ya mwisho”, lakini kamwe hili halitarajiwi haswa kwa mustakbali wa karibuni kwa sababu zifuatazo:

A – Hotuba ya Trump mnamo 9/6/2017 iliyotajwa juu haikuacha nafasi kwa Qatar kulegeza msimamo kwa sababu alilizungumzia hilo:

“Taifa la Qatar kwa bahati mbaya, kihistoria limekuwa mfadhili wa ugaidi kwa kiwango kikubwa. Na kwa kutokea kwa kongamano hilo, mataifa yalikuja pamoja na kusema nami kuhusu kuikabili Qatar juu ya tabia yake hii. Kwa hivyo tulikuwa na uamuzi wa kufanya: Je, tufuate barabara sahali au hatimaye tuchukue kitendo kigumu lakini kinacho stahili? Lazima tukomeshe ufadhili wa ugaidi. Nimeamua pamoja na waziri wa kigeni Rex Tillerson, magenerali wetu wakuu na wanajeshi, wakati umewadia kutoa wito kwa Qatar to kukomesha ufadhili wake…” (Al-Youm As-Sabi’,9/6/2017)

Inajulikana kuwa Qatar haitungi siasa zake yenyewe, bali Uingereza huitungia, na siasa ya sasa ya Uingereza haikabiliana na Amerika hadharani, haswa katika hatua ya sasa ambayo ni hatua ya kujitoa katika Umoja wa Ulaya; inajaribu kuwa karibu nayo hata juu ya sakafu.

B – Mawazo ya Trump ni kama ya mfanyi biashara, upande wa kifedha ndio ulio na athari zaidi. Ikiwa Qatar italipa kinachomvutia Trump, huenda akamuagiza Salman kulegeza msimamo! Mtafiti wa kiamerika Jonathan Kristol mshirika katika Taasisi ya Siasa ya Kiulimwengu (World Policy Institute), alisema: “Pesa alizonazo Donald Trump ndani ya ikulu ya white

Endelea Uk..18

house ndio ufunguo wa mgogoro wa kukatwa kwa Qatar na Saudi, Imarati na Bahrain", alifafanua katika makala yake kuwa njia pekee kwa Qatar kushinda shinikizo la kidiplomasia na la kiuchumi la Saudi ni kupitia Amerika kuingilia kati pamoja na vibaraka wake wa kisaudi kwa njia ya pesa, kulingana na CNN…" (Arabi 21, 6/6/2017).

Yaani, mtazamo unaotarajiwa zaidi ni kuwa kuna suluhisho kupitia pesa za Qatar au kujisalimisha kwa Qatar! Na twasema kuwa kinacho tarajiwa zaidi ni kuwa Uingereza itakapo amini kuwa maslahi yake wakati wowote yanahitaji kujiondoa kwa Qatar kutoka kwa jumuia (ya Ghuba), itajiondoa, na ikiwa yanahitaji kubakia kwake, itabakia kwa sababu Qatar haiendeshi siasa yake wenyewe, lakini Uingereza ndio yenye kuendesha!

7 – Kutamatisha, hakuna kheri yoyote inayotarajiwa kutoka kwa vibaraka wa Amerika nchini Saudi Arabia, Misri na wale waliowafuata katika kadhia hii ya kukata mahusiano; wamezisalimisha biladi za kiislamu na watu wake kwa maadui wa Uislamu na Waislamu kwa badali ya kubakisha viti vyao vya utawala, vyenye miguu mibovu ambayo leo au kesho yaweza kuvunjika. Zaidi ya hayo, hakuna kheri yoyote inayo tarajiwa kutoka kwa Qatar inayo endeshwa nyuma ya Uingereza kupewa miradi ya uharibifu dhidi ya Waislamu; imeipatia Amerika kambi kubwa zaidi ambayo ndege zake hurukia kwenda kuua na kuangamiza watoto wa Waislamu Syria na Iraq na kuharibu majumba yao. Pia inaunga mkono kuhifadhi amani na dola ya kiyahudi; imeifanya Hamas kulegeza msimamo kwa kuiga Fatah katika kuweka miungano. Zaidi ya hayo, imeziathiri baadhi ya harakati za Syria kwa pesa zake za sumu kwa kuzishurutisha kuingia katika majadiliano na serikali ya kihalifu huko. Inawahadaa wale walio na mitazamo ya kiislamu na kuwaghuri kwa pesa na makao ili kuwavutia kulegeza msimamo na kubadilisha mielekeo na fikra zao. Yote haya ni katika jukumu lake ovu ililochorewa na Uingereza. Kwa hivyo ni uchali na karibu na uhaini kuihurumia serikali hii au nyengineyo kwa kisingizo cha (qaida ya) 'la khafifu katika madhara mawili'; kadhia za umma hazipimwi katika mizani ya madhara na madhara khafifu, bali hupimwa kwa mizani ya haki na batil. Watoto wa umma lazima wapinge serikali hizi zinazofanya khiana kwa Allah (swt), Mtume wake (saw) na kwa waumini, na hawana budi kufanya kazi na wafanyi kazi mukhlisina kuzing'oa na kuasisi dola yao; bishara ya Mtume wao mtukufu (saw); Khilafah Rashidah itakayo simamia mambo yao katika usalama na amani majumbani mwao, njiani na safarini mwao, itakayo leta izza kwa Uislamu na Waislamu na itakayo dhalilisha makafiri wakoloni, na hapo ndipo Trump na wapambe wake na vibaraka wake watakapo fikwa na janga miilini mwao na majumbani mwao.

وَاللَّهُ غَالِبٌ عَلَى أَمْرِهِ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ

**"Na Allah ni Mshindi juu ya jambo lake lakini wengi watu hawajui" [Yusuf: 21]**

**16 Ramadhan 1438 AH**
**11/6/2017 CE**



Email: uqab@hizb.or.ke